SHIRIKA LA RELI TANZANIA

Jarida la

RELI NA MATUKIO

Toleo namba 22, Julai 2022

Habari | Makala | Matukio | Elimu | Picha

# RAIS SAMIA ASHUHUDIA UTIAJI SAINI WA MIKATABA MIWILI KATIKA SEKTA YA RELI NCHINI



Mkurugenzi Mkuu wa TRC Masanja Kadogosa (wa pili kulia) na wawakilishi wa kampuni ya Yapi Merkezi (kushoto), wakisaini mkataba wa ujenzi wa reli ya kisasa - SGR Tabora - Isaka katika ukumbi wa mikutano Ikulu jijini Dar es Salaam Julai 4, 2022

Na Mwandhishi wetu

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan ameshuhudia utiaji saini wa mikataba miwili ambayo ni mkataba wa ujenzi wa reli ya kisasa – SGR kipande cha Tabora – Isaka pamoja na mkataba wa mafunzo kwa vitendo kwa watumishishi wa Shirika la Reli Tanzania - TRC, Ikulu jijini Dar es Salaam Julai 4, 2022.

Mkataba wa ujenzi wa reli ya kisasa kipande cha Tabora – Isaka umesainiwa kati ya TRC na kampuni ya Yapi Merkezi kutoka nchini Uturuki ikiwa ni ukamilishaji wa sehemu ya ujenzi wa reli ya kisasa awamu ya kwanza kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza yenye vipande vitano.



Mkurugenzi Mkuu TRC Masanja Kadogosa (wa pili kulia) na wawakilishi wa Korea Railways (kushoto), wakisaini mkataba wa mafunzo kwa vitendo kwaajili ya watumishi watakaosimamia reli ya kisasa - SGR, Ikulu jijini Dar es Salaam Julai 4, 2022

Inaendelea Uk. 2

# RAIS SAMIA ASHUHUDIA UTIAJI SAINI WA MIKATABA MIWILI KATIKA SEKTA YA RELI NCHINI

Inatoka Uk. 1

Mkataba wa mafunzo kwa vitendo umesainiwa kati ya TRC na kampuni ya Korea Railways kutoka nchini Korea ukiwa na lengo la kuwapa mafunzo watumishi wa Shirika katika kipindi cha ujenzi na uendeshaji mara baada ya reli ya kisasa kukamilika na kukabidhiwa kwa TRC.

Aidha, kipande cha Tabora hadi Isaka kina jumla ya kilomita 165 ambapo kilomita 130 ni njia kuu na kilomita 35 ni njia za kupishania. Thamani ya mkataba wa ujenzi ni Dola za kimarekani milioni 900.1 sawa na fedha za kitanzania trilioni 2.094, muda wa utekelezaji ni miezi 42 ikijumlisha muda wa majaribio wa miezi 6

Hafla ya utiaji saini mikataba hiyo imehudhuriwa na viongozi wa Serikali akiwemo Waziri Mkuu, Katibu Mkuu Kiongozi, viongozi wa dini, wakuu wa majeshi, mawaziri na naibu mawaziri, makatibu wakuu, wakuu wamikoa, wakuu wa wilaya, uongozi wa wizara pamoja na uongozi na wafanyakazi wa Shirika la Reli.

Rais Samia amesema kuwa mikataba iliyosainiwa ni muhimu katika kuendeleza mradi wa SGR ambao kwa kiasi kikubwa unakwenda kuleta maendeleo ya kiuchumi pamoja na kupunguza utegemezi wa wataalamu wa sekta ya reli kutoka nje.

"Mikataba hii ina umuhimu wa kipekee kwakuwa inakamilisha awamu ya kwanza ya reli yetu ya kisasa kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza na kuanza matayarisho ya kuwajengea uwezo watanzania wa kuendesha na kuisimamia reli yetu badala ya kutegemea wataalamu kutoka nje" alisema Rais Samia

Mhe. Samia amesisitiza kuwa reli ya kisasa itaunganisha mikoa 9 ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Dodoma, Singida, Tabora, Simiyu na Mwanza lakini pia itaziunganisha nchi za jirani za Uganda, Burundi, Rwanda, DRC, Sudani ya Kusini na nchi nyingine za Afrika. Rais Samia ameipongeza Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Shirika la Reli, Wakandarasi na washauri kwa usimamizi mzuri wa mradi wa SGR.



Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akihutubia wakati wa hafla ya utiaji saini mkataba wa ujenzi wa reli ya kisasa Tabora - Isaka na mkataba wa mafunzo kwa vitendo, Ikulu jijini Dar es Salaam Julai 4, 2022.



Masanja Kungu Kadogosa, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania akitoa taarifa ya maendeleo ya mradi wa SGR na mkataba wa ujenzi wa reli ya kisasa Tabora - Isaka na mkataba wa mafunzo kwa vitendo, Ikulu jijini Dar es Salaam Julai 4, 2022.



Baadhi ya wageni na viongozi wa Serikali wakifuatilia hotuba ya Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati wa hafla ya utiaji saini mkataba wa ujenzi wa reli ya kisasa Tabora - Isaka na mkataba wa mafunzo kwa vitendo, Ikulu jijini Dar es Salaam Julai 4, 2022.

Inaendelea Uk. 3

# RAIS SAMIA ASHUHUDIA UTIAJI SAINI WA MIKATABA MIWILI KATIKA SEKTA YA RELI NCHINI




Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi Bwana Gabriel Migire (wa sita kulia) akiwa katika picha ya pamoja na Menejimenti ya TRC mara baada ya hafla ya utiaji saini mkataba wa ujenzi wa reli ya kisasa Tabora - Isaka na mkataba wa mafunzo kwa vitendo Ikulu jijini Dar es Salaam Julai 4, 2022.

Inatoka Uk. 2

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Masanja Kungu Kadogosa ameeleza kuwa thamani ya uwekezaji wa ujenzi wa reli ya kisasa umefikia trilioni 16 kwa awamu ya kwanza ya Dar es salaam hadi Mwanza na serikali hadi sasa imelipa malipo yenye jumla ya shilingi trilioni 6.4 kwa kazi yote iliyotekelezwa na kuhakikiwa ubora wake.

Kadogosa amemshukuru Rais Samia kwa ujasiri wa kuendeleza mradi wa SGR kwasababu unatumia fedha nyingi na kuongeza kuwa mradi wa SGR utaleta manufaa kwa vizazi vya sasa na vijavyo na kutambua mchango mkubwa uliofanywa na Mhe. Samia akiwa Makamu wa Rais na sasa akiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.




Baadhi ya wageni waliohudhuria hafla ya utiaji saini mkataba wa ujenzi wa reli ya kisasa Tabora - Isaka na mkataba wa Mafunzo kwa vitendo wakifuatilia taarifa ya Mkurugenzi Mkuu TRC Masanja Kadogosa katika ukumbi wa mikutano Ikulu jijini Dar es Salaam, Julai 2022.

# TRC YASHIRIKI MAONESHO YA SABASABA JIJINI DAR ES SALAAM

**Na Mwandishi wetu**

Shirika la Reli Tanzania - TRC limeshiriki maonesho ya Kimataifa ya biashara yanayoendelea katika viwanja vya Sabasaba jijini Dar es Salaam kuanzia Juni 28 hadi Julai 13, 2022.

Maonesho ya Sabasaba yana lengo la kuwakutanisha watoa huduma, wauza bidhaa na wateja na watumiaji wa huduma au bidhaa ambapo TRC imedhamiria kutoa elimu kwa wananchi kuhusu huduma mbalimbali zitolewazo na shirika ikiwemo usafirishaji wa mizigo na abiria, ujenzi na maendeleo ya miundombinu ya reli ikiwemo ujenzi wa reli ya kisasa - SGR na uboreshaji wa reli ya zamani (MGR).



Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhe. Atupele Mwakibete (wa pili kushoto) akisikiliza maelezo kuhusu mifumo mbalimbali ya mawasiliano ya treni alipotembelea banda la TRC katika maonesho ya 46 ya Kimataifa ya Biashara katika viwanja vya Mwl. Nyerere barabara ya Kilwa jijini Dar es Salaam Julai 2022

Ushiriki wa TRC katika maonesho hayo yanalenga katika kupanua wigo wa kibiashara kati ya shirika na makampuni mbalimbali,wadau na wananchi kwa ujumla.

Katika banda la TRC wananchi wamepata huduma za kukata tiketi, kufahamu mifumo ya reli ya zamani (MGR) na ile ya SGR itakayotumia nishati ya umeme, elimu kuhusu historia ya TRC na maendeleo ya mradi wa SGR kupitia video, vipeperushi na majarida.

Aidha, maonesho ya Sabasaba yameendelea kuleta hamasa kwa wananchi wanaotembelea banda la TRC kwani wengi wao wanaonesha matamanio ya kuanza kwa shughuli za uendeshaji wa reli ya kisasa SGR.

"Tunashukuru sana kwa ujenzi wa SGR, tunatamani uishe haraka ili tuweze kufanya biashara kwa wepesi, mimi kama mfanyabiashara itanisaidia sana" alisema bwana Tahir Othman alipotembelea banda la TRC.

Naye Bwana Moses Mwakyanjala, Mkazi wa Ukonga jijini Dar es Salaam amesema "usafiri wa reli ni mzuri sana hasa kwa miji mikubwa kama Dar es Salaam, hivyo basi ningependa TRC iboreshe miundombinu ya treni za mijini, vituo vya kushusha na kupakiza abiria na uwepo wa mawakala wa kukata tiketi za treni ili kuboresha huduma na kuongeza mapato kwa nchi"

Wakati maonesho haya yakiendelea viongozi mbalimbali wametembelea banda la Shirika la Reli Tanzania akiwemo Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhe. Atupele Bwakibete, ambaye ameipongeza TRC kwa kujipanga vizuri na kuwaelezea wananchi wanaopita bandani kuhusu shughuli

Inaendelea Uk. 5

# TRC YASHIRIKI MAONESHO YA SABASABA JIJINI DAR ES SALAAM



Baadhi ya wananchi wakipata maelezo kutoka kwa Mhandisi Moga Masunga (kushoto) kuhusu maendeleo ya mradi wa SGR katika banda la TRC lililopo viwanja vya Mwl. Nyerere barabara ya Kilwa jijini Dar es Salaam, Julai 2022



Wanafunzi wa shule ya awali na msingi ya Agape wakijiandaa kupanda Kiberenge walipotembelea banda la TRC katika viwanja vya Mwl. Nyerere barabara ya Kilwa jijini Dar es Salaam, Julai 2022

Inatoka uk. 4

zinazofanywa na TRC ikiwemo mradi wa kimkati wa SGR pamoja na usafirishaji wa Abiria na mizigo kwa reli ya Kati pamoja na reli ya Kaskazini

Mhe Atupele ameongeza kuwa kuwa “mradi wa kimkakati wa SGR imefikia pazuri kuanzia awamu ya kwanza ambayo ni Dar es Salaam - Morogoro, Morogoro - Makutupora, Makutupora - Tabora pamoja na Isaka - Mwanza na hivi karibuni kitaanza kujengwa kipande cha Tabora - Isaka" Mwakibete.

Serikali inategemea kupokea behewa na vichwa vya Treni ya kisasa Agosti 2022 na majaribio yataanza kufanyika mwezi Septemba 2022 katika kipande cha Dar es salaam hadi Morogoro.

"Wananchi wategemee mambo mazuri kuanzia mwezi wa tisa kama nilivyoelezea Bungeni kuhusu majaribio ya kipande cha Dar es Salaam Hadi Morogoro" ameongeza Mheshimiwa Mwakibete.

Viongozi wengine waliotembela banda la TRC ni pamoja na Balozi wa Japani nchini Tanzania Yasushi Misawa, Wanafunzi wa Shule ya Msingi ya Agape iliyopo Mbagala Jijini Dar Es Salaam na watu mbali mbali.



Barozi wa Japan Nchini Tanzania Bw. Yasushi Misawa (aliyevaa suti) akisikiliza maelezo kutoka kwa Mhandisi Moga Masunga (kulia) kuhusu uboreshaji wa reli ya kati alipotembelea banda la TRC katika maonesho ya 46 ya Kimataifa ya Biashara katika viwanja vya Mwl. Nyerere barabara ya Kilwa jijini Dar es Salaam Julai 2022

# TRC YAENDELEA NA ZOEZI LA FIDIA KUPISHA MRADI WA SGR MWANZA - ISAKA



Mhasibu kutoka Shirika la Reli Tanzania Bwana Nassor Said (kulia) akiendelea na zoezi la kukabidhi hundi za malipo ya fidia kwa wananchi wa kijiji cha Nyamatala Misungwi mkoani Mwanza, Juni 2022.

**Na Mwandishi wetu**

Shirika la Reli Tanzania – TRC limeendelea na zoezi la malipo ya fidia kwa wanachi waliotwaliwa maeneo yao kupisha mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa mkoani Shinyanga na Mwanza, hivi karibuni Juni 2022.

Malipo ya fidia yanaendelea kwa lengo la kutwaa ardhi kwaajili ya kukabidhi eneo kwa mkandarasi wa mradi wa SGR kipande cha tano Mwanza – Isaka chenye urefu wa KM 361.

Zoezi limefanyika katika vijiji vya Lugembe, Sumbigu na Bukigi mkoani Shinyanga na vijiji vya Mwagala na Nyamatala Misungwi mkoani Mwanza ambapo takribani hundi 302 zimekabidhiwa kwa wahusika.

Mwenyekiti wa kijiji cha Sumbigu bwana Simon Masunga amezungumzia kuhusu mradi wa SGR kwa kusema kuwa "Zoezi tumelipokea, mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa nao unaendela hakuna malalmiko yoyote na zoezi la fidia limefanikiwa katika kijiji changu"

Baadhi ya wananchi waliopokea fidia zao wamefu rahishwa na hatua ya Serikali ya kulipa fidia kwa wakati. Pia wamemshukuru Mhe. Rais Samia Suluhu, watumishi wa Serikali na benki kwa kukamilisha zoezi la fidia katika maeneo hayo.

Aidha, mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa Mwanza – Isaka umefikia 6.83% kazi kubwa zikiwa ni ujenzi wa tuta, vivuko, makalavati na madaraja. Kasi ya ujenzi inaenda sambamba na upatikanaji wa ardhi ambayo kwa kiasi kikubwa Serikali imefanikisha kukabidhi eneo kwa mkandarasi kuendelea na ujenzi.



Maafisa wa Shirika la Reli Tanzania (waliovaa vizibao) na Afisa Mtendaji wa kijiji cha Sumbigu wakiandaa nyaraka za malipo ya fidia kwa wananchi waliotwaliwa maeneo kupisha mradi wa SGR mkoani Shinyanga Juni 2022.

# UNUNUZI WA INJINI NA BEHEWA ZA ABIRIA NA MIZIGO KWA MATUMIZI YA RELI YA KISASA - SGR



Muonekano wa seti ya treni ya kisasa aina ya EMU itakazotumika kwaajili ya kubeba abiria katika reli ya kisasa - SGR

**Na Mwandishi wetu**

Shirika la Reli Tanzania - TRC limetoa ufafanuzi juu ya ununuzi wa injini na behewa za abiria na mizigo kwa matumizi ya reli ya kisasa - SGR kwenye mkutano wa waandishi wa habari uliofanyika katika ukumbi wa mikutano TRC jijini Dar es Salaam Juni, 2022.

Mkuu wa Kitengo cha Habari na Uhusiano TRC Bi. Jamila Mbarouk ameeleza kuwa TRC inafanya manunuzi ya behewa za mizigo, behewa za abiria, seti za treni za kisasa pamoja na vichwa vya treni ya umeme kwa mgawanyo wa awamu mbili.

Bi. Jamila alisema kuwa awamu ya kwanza ya ununuzi wa vifaa vya uendeshaji wa mtandao wa reli ya kisasa awamu ya kwanza Dar es Salaam - Mwanza yenye urefu wa kilometa 1,219 ambapo muda wa manunuzi ni miezi 36 hadi 48, pia manunuzi ya pili ni ya vichwa na behewa kwaajili ya majaribio na uendeshaji wa awali ambapo muda wa manunuzi ni miezi 9.

"Manunuzi yamefanyika kwa kuzingatia Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011, pamoja na marekebisho ya mwaka 2016, kanuni za mwaka 2013 na marekebisho ya kanuni ya mwaka 2016" alisema Bi. Jamila.

idha, Bi. Jamila alieleza kuwa katika kuhakikisha uendeshaji wa awali unaanza mara baada ya majaribio, TRC ilisaini mkataba wa muda mfupi wa ununuzi wa vichwa vya treni ya umeme viwili na behewa 30 za abiria vilivyotakiwa kufanyiwa ukarabati kutoka kampuni ya Eurowagon ya nchini Uturuki.

Hata hivyo Bi. Jamila aliongeza kuwa kampuni ya Eurowagon ilishindwa kutimiza matakwa ya mkataba huo ambao ulitakiwa kukamilika mnamo mwezi Novemba, 2021 na kupelekea kusitishwa kwa mkataba huo Februari 2022.

"Ujenzi kipande cha kwanza Dar es Salaam - Morogoro upo hatua ya mwisho, hivyo TRC iliamua kusitisha mkataba kwa barua mnamo tarehe 25, Februari , 2022" alisema Bi. Jamila

Vilevile Bi. Jamila alisisitiza kuwa TRC inaendelea na jukumu la kumalizia ukarabati bila gharama na vifaa vinatarajiwa kukamilika mwezi Agosti 2022.

Naye Mkurugenzi wa Ujenzi na Miundombinu Mhandisi Machibya Masanja alisema kuwa TRC ilisaini mikataba ya manunuzi ya behewa mpya 1,430 za mizigo kutoka kampuni ya CRRC ya nchini China, behewa mpya za abiria 59 kutoka kampuni ya Sung Shin Rolling Stock Technology Limited

**Inaendelea Uk. 8**

# UNUNUZI WA INJINI NA BEHEWA ZA ABIRIA NA MIZIGO KWA MATUMIZI YA RELI YA KISASA - SGR



Muonekano wa ndani wa moja kati ya behewa za abiria za reli ya kisasa - SGR

Inatoka UK. 7

kutoka nchini Korea Kusini, seti 10 mpya za treni za kisasa zenye behewa 80 na vichwa 17 vipya vinavyotumia nishati ya umeme kutoka kampuni ya Hyundai Rotem ya Korea Kusini kwaajili ya uendeshaji wa reli ya SGR.

"Gharama ya mikataba ni shilingi Trilioni 1.18 na ipo kwenye hatua mbalimbali za utekelezaji" alisema Mhandisi Machibya.



Mkuu wa Kitengo cha Habari na Uhusiano TRC Bi. Jamila Mbarouk akifafanua kuhusu mikataba ya ununuzi wa behewa na vichwa vya treni za SGR katika mkutano na waandishi wa habari TRC makao makuu jijini Dar es Salaam, Juni 2022.



Muonekano wa ndani wa moja kati ya behewa za abiria za reli ya kisasa - SGR



Mkurugenzi wa Miundombinu na Ujenzi TRC Mhandisi Machibya Masanja akizungumzia kuhusu maendeleo ya mradi wa SGR qKti wa mkutano wa waandishi wa habari, makao makuu TRC Dar es Salaam Juni, 2022.

Mhandisi Machibya alieleza kuwa mikataba hiyo ya ununuzi imetolewa katika kampuni mbalimbali ambazo zilitaja bei nzuri ya manunuzi.

Pia Mhandisi Machibya alisema kuwa ujenzi wa SGR unajengwa kwa ufanisi na kuhakikisha usalama kwa wananchi kwa kujenga vivuko katika njia ya reli ikiwemo kivuko cha wanyama, binadamu na vyombo vya usafiri.

"Usanifu na ujenzi wa SGR tumezingatia mazingira halisi ya mtanzania" alisema Mhandisi Machibya.

Ujenzi wa SGR kwa awamu ya kwanza Dar es Salaam - Mwanza unaendelea vema na mchakato wa manunuzi ya mkandarasi wa ujenzi wa awamu ya pili kwa kipande cha Tabora - Kigoma unaendelea.